



KLABU ZA HAKI ZA BINADAMU: THBUB INAVYOJENGA KIZAZI CHA MABALOZI WA HAKI NCHINI

Kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru Bw. Wazo Michael Mwang'onda akizindua Klabu ya Haki za Binadamu katika Shule ya Sekondari Hamida Alqassim iliyopo Manispaa ya Lindi Mkoa wa Lindi Mei 2, 2026.

Katika safari ya kujenga taifa linalozingatia haki za binadamu na utawala bora, elimu kwa vijana imeendelea kuwa moja ya nguzo muhimu za mabadiliko ya kijamii. Kwa kutambua nafasi hiyo, Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (THBUB) imeamua kuwekeza katika programu ya Klabu za Haki za Binadamu katika shule za msingi, sekondari pamoja na vyo vya kati na vikuu ili kuwajengea wanafunzi maarifa, stadi na maadili yatakayowawezesha kuwa mabalozi wa haki za binadamu katika jamii zao.

Juhudi hizo zimeanza kuonesha mafanikio makubwa, ambapo zaidi ya wanafunzi 5,000 kutoka shule na vyo mbalimbali nchini wamenufaika moja kwa moja na mafunzo ya haki za binadamu na utawala bora. Sambamba na hilo, zaidi ya klabu 300 za haki za binadamu zimeanzishwa katika shule na taasisi za elimu, zikiwa jukwaa muhimu kwa wanafunzi kujifunza, kujadili na kuhamasisha masuala ya haki za binadamu, utawala bora na namna ya kupinga vitendo vya ukatili miongoni mwao na jamii inayowazunguka.

Mafanikio hayo yanaakisi dhamira ya THBUB ya kujenga kizazi kinachotambua haki zake, kutekeleza wajibu wake na kushiriki kikamilifu katika kuimarisha ustawi wa wananchi.

Mkurugenzi wa Elimu kwa Umma, Mawasiliano, Tafiti na Nyaraka wa THBUB, Bi. Monica Mnanka, ameeleza kuwa lengo la kuanzishwa kwa klabu hizo ni kuwajengea uwezo wanafunzi hao ili waweze kuwa mabalozi wa haki za binadamu katika jamii zao.



Kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru Bw. Wazo Michael Mwang'onda akizindua Klabu ya Haki za Binadamu katika Shule ya Sekondari Hamida Alqassim iliyopo Manispaa ya Lindi Mkoa wa Lindi Mei 2, 2026

Akitoa takwimu ya idadi ya klabu za haki za binadamu nchini, Bi. Mnanka amesema katika kipindi cha robo ya nne ya mwaka (April mpaka Juni 2026) Jumla ya Klabu 15 zilifunguliwa katika Mikoa ya Shinyanga, Mtwara, Lindi, Dar es Salaam, Ruvuma, Kigoma na Zanzibar. Hivyo, kufanya idadi jumla ya klabu za haki za binadamu nchini kuwa 375.

Wataalamu wa elimu wanaeleza kuwa Klabu za Haki za Binadamu zinasaidia kuwajengea wanafunzi kuwa raia wema na wenye ujasiri wa kuripoti vitendo vya ukatili na unyanyasaji wanapovishuhudia katika jamii.

UTANGULIZI



Bw. Patience Ntwina
Katibu Mtendaji-THBUB

Ndugu msomaji, Napenda kukukaribisha kusoma Jarida la Sauti ya Haki "Voice of Haki" la robo ya nne kwa Mwaka wa fedha 2025/2026. Jarida hili linaangazia baadhi ya shughuli na mafanikio yali-yopatikana katika utekelezaji wa majukumu ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (THBUB). Miongoni mwa habari zilizopewa kipaumbele ni elimu ya haki za binadamu kupitia klabu za haki za binadamu, mafunzo na ushiriki katika madhimisho ya kitaifa, hatua ambazo zinaendelea kuongeza uelewa wa wananchi kuhusu masuala ya haki, na misingi ya utawala bora. Mengine yaliyoangaziwa ni pamoja na mchango wa Kitengo cha Taasisi za Haki Jinai katika kushughulikia malalamiko ya wananchi;

mafunzo kwa watumishi wa THBUB katika kuimarisha utendaji kazi; ushirikiano wa THBUB na taasisi za kikanda pamoja na mchango wa THBUB katika kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi. Ninatambua kuwa utekelezaji wa majukumu ya THBUB hauwezi kufanikiwa bila ushirikiano na wadau mbalimbali. Hivyo, nitumie fursa hii kuwashukuru watumishi wote wa THBUB, Serikali, taasisi za Umma na binafsi, washirika wa maendeleo na wananchi kwa ushirikiano na mchango wao katika kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya THBUB kwa mwaka wa fedha 2025/2026. Ninatoa rai kwa wadau wote kuendelea kushirikiana na THBUB katika mwaka wa fedha 2026/2027.

KAMATI YA UHARIRI

Mwenyekiti:
Monica Mnanka

Mhariri:

Zawadi Msalla
Mhariri Msaidizi:
Nuru Mfaume

Wajumbe:

Mwashamba Juma
Tumaini Obel
Farida Ruben

USANIFU

Baraka Mgulu
Nuru Mfaume

MAWASILIANO

Makole,
Jengo PSSF
S.L.P 1049 DODOMA,
Tanzania
Simu: +255 738 279744
Barua Pepe:
www.chragg.go.tz



YALIYOMO

KLABU ZA HAKI ZA BINADAMU: THBUB INANYOJENGA KIZAZI CHA MABALOZI WA HAKI NCHINI. UK 1

THBUB YASHIRIKI KIKAO CHA 87 CHA TUME AFRIKA YA HAKI ZA BINADAMU NA WATU. UK 3.

THBUB YAWAFIKIA ZAIDI YA WANANCHI 89,000. UK 4.

MOBILE CLINIC YA OFISI YA RAIS YAWAFIKIA WATUMISHI THBUB. UK 5

WATUMISHI WA UMMA WATAKIWA KUIMARISHA UTENDAJI KAZI KWA MANUFAA YA WANANCHI. UK 6.

KITENGO CHA TAASISI ZA HAKI JINAI KUIMARISHA UTOAJI HAKI. UK 7.

THBUB Yawekeza kwa watumishi wapya ili kuimarisha huduma bora kwa wananchi. UK 8.

THBUB Yasisitiza ulinzi wa haki za binadamu katika usimamizi wa rasilimali za bahari. UK 9.

BUSTANI YA MITI YAZINDULIWA WIKI YA MAZINGIRA. UK 10.

HABARI PICHA UK 11,12,13, 14,& 15.

THBUB YASHIRIKI KIKAO CHA 87 CHA TUME YA AFRIKA YA HAKI ZA BINADAMU NA WATU.



Mkurugenzi Idara ya Huduma za Kisheria wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora Bi. Ellen Rwijage (katikati) akiwa katika kikao cha 87 cha Tume ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu kilichofanyika Jijini Banjul, Nchini Gambia Julai 11, 2026 .

Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (THBUB) imeshiriki Kikao cha 87 cha Tume ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu (African Commission on Human and Peoples' Rights – ACHPR), kilichofanyika Jijini Banjul, nchini Gambia kuanzia tarehe 11 hadi 20 Mei, 2026.

Kikao hicho kiliwakutanisha wadau mbalimbali kutoka nchi za Afrika kujadili masuala yanayohusu ulinzi na ukuzaji wa haki za binadamu, utawala bora, utawala wa sheria pamoja na utekelezaji wa mikataba ya kikanda inayolenga kuimarisha haki na maendeleo ya wananchi barani Afrika.

Akizungumza kuhusu ushiriki wa THBUB katika kikao hicho, Mkurugenzi wa Huduma za Sheria katika THBUB Bi. Ellen Rwijage aliyeshiriki kikao hicho, amesema kuwa vikao vya Tume ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu vinatoa jukwaa muhimu kwa taasisi za kitaifa za haki za binadamu, Serikali, mashirika ya kiraia, wataalamu wa sheria na wadau wengine kubadilishana uzoefu, kujifunza mbinu bora na kujadili changamoto zinazojitokeza katika kulinda na kukuza haki za binadamu.

Bi. Rwijage amebainisha kuwa, kupitia mijadala hiyo, nchi wanachama hupata fursa ya kutathmini maendeleo yaliyofikiwa katika utekelezaji wa wajibu wao wa kitaifa na kimataifa.

"Vikao hivi ni muhimu sana kwa sababu vinatupa nafasi ya kujadili masuala mbalimbali yanayohusu haki za binadamu, kubadilishana uzoefu na kuimarisha mifumo ya haki na utawala bora ambayo ni maeneo muhimu yanayochangia utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050," amesema Bi. Rwijage.

Aidha, Bi. Rwijage amesema kuwa ajenda zilizojadiliwa katika kikao hicho zinaendana na malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050, ambayo inaweza msisitizo katika kujenga taifa lenye misingi imara ya utawala bora na ulinzi wa haki za binadamu. Ameeleza kuwa maendeleo endelevu hayawezi kufikiwa bila kuwepo kwa taasisi imara zinazoheshimu haki za binadamu na kuhakikisha wananchi wanashiriki kikamilifu katika maendeleo ya nchi yao.

Ushiriki wa THBUB katika Kikao cha 87 cha Tume ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu ni sehemu ya utekelezaji wa wajibu wa Tanzania katika kukuza na kulinda haki za binadamu, pamoja na kuimarisha misingi ya utawala bora kupitia ushirikiano wa kikanda na kubadilishana uzoefu unaochangia maendeleo na ustawi wa wananchi.

THBUB YAWAFIKIA ZAIDI YA WANANCHI 89,000 KUPITIA ELIMU YA HAKI ZA BINADAMU

39,129 na vitabu 200 vya elimu vikisambazwa kwa wananchi ili kuongeza uelewa kuhusu haki za binadamu, utawala bora na namna ya kuwasilisha malalamiko THBUB.

Aidha, THBUB ilirusha vipindi 79 vya elimu kupitia redio na televisheni, hatua iliyochangia kuwafikia wananchi wengi zaidi nchini.

THBUB itaendelea kutumia teknolojia na majukwaa mbalimbali kuhakikisha elimu ya haki za binadamu inawafikia Watanzania wengi zaidi.

Pia, Bi. Mnanka amesema THBUB imeendelea kuwekeza katika elimu ya haki za binadamu kwa kutoa mafunzo kwa zaidi ya washiriki 9,300 kutoka makundi mbalimbali ya jamii nchini katika mwaka wa fedha 2025/2026.

Akitoa takwimu ya walionufaika na mafunzo hayo, Bi. Mnanka ametaja makundi hayo kuwa ni pamoja na askari wa Jeshi la Polisi 827, waandishi wa habari 324, madiwani 60, wanafunzi zaidi ya 8,000 na walimu 121 kutoka vyuo vikuu 09 pamoja na taasisi za elimu ya kati.

Mafunzo hayo yalilenga kuongeza uelewa kuhusu haki za binadamu na misingi ya utawala bora.

“.....kuwajengea uwezo makundi mbalimbali katika jamii ni hatua muhimu katika kuimarisha utamaduni wa kuheshimu haki za binadamu na misingi ya utawala bora.....” amesema Bi. Mnanka.

Mkurugenzi Elimu kwa Umma, Mawasiliano, Utafiti na Nyaraka wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora Bi. Monica Mnanka akizungumza na vyombo vya habari Jijini Dar es Salaam Juni 28, 2026.

Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (THBUB) imeendelea kuimarisha uelewa wa wananchi kuhusu haki za binadamu na misingi ya utawala bora kwa kuwafikia zaidi ya wananchi 89,000 kupitia njia mbalimbali za utoaji elimu katika mwaka wa fedha 2025/2026.

Elimu hiyo ilitolewa kupitia mafunzo kwa makundi mbalimbali ya jamii, vipindi vya redio na televisheni, mitandao ya kijamii, huduma ya ujumbe mfupi wa simu (Bulk SMS) pamoja na usambazaji wa vipeperushi na machapisho ya elimu.

Taarifa hiyo imetolewa na Msemaji wa THBUB ambaye pia ni Mkurugenzi wa Elimu kwa Umma, Mawasiliano, Utafiti na Nyaraka wakati akiongea na vyombo vya habari katika viwanja vya Maonesho ya Kimataifa ya Biashara saba saba Juni 28, 2026

Bi. Mnanka amesema katika kipindi hicho, wananchi zaidi ya 80,000 walifikishiwa ujumbe wa elimu kupitia simu za mkononi, huku vipeperushi



Wanafunzi wa Chuo cha Mipango wakifuatilia maeleze kuhusu majukumu ya THBUB kutoka kwa Afisa wa THBUB (hayupo pichani) wakati walipotembelea banda la THBUB katika wiki ya Utumishi wa Umma Viwanja vya Chinangali Jijini Dodoma Juni 22, 2026.

MOBILE CLINIC OFISI YA RAIS YAWAFIKIA WATUMISHI WA THBUB



Jumla ya Watumishi 61 wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (THBUB), wamenufaika na mafunzo maalum ya e-utendaji yanayojulikana kama Mobile Clinic yaliyolenga kuimarisha utendaji kazi, maadili ya utumishi wa umma pamoja na mshikamano kazini.

Mafunzo hayo yametolewa na Ofisi ya Rais – Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora (OR-MUUUB) Aprili 29, 2026 katika Ukumbi wa Jakaya Kikwete ikiwa ni zoezi linalofanyika kwa Taasisi zote za Umma nchini.

Akizungumza kwa niaba ya Katibu Mkuu Ofisi ya Rais-Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Bw. Oswin Henry Mkinga alisema mafunzo hayo yanawakumbusha watumishi umuhimu wa uzalendo, kufanya kazi kwa bidii, kujituma na kudumisha upendo na ushirikiano katika utekelezaji wa majukumu yao ya kila siku.

Aidha, msisitizo umewekwa katika kuondokana na tabia zisizojenga taasisi kama vile majungu, makundi na kujipendekeza kwa viongozi, badala yake amesisitiza kujenga utamaduni wa kuheshimiana, kushirikiana na kuinuana katika utumishi wa umma.

"Watumishi ni kiungo muhimu kati ya Serikali na wananchi, hivyo mnapaswa kutekeleza majukumu yenu kwa uadilifu, uwajibikaji na weledi wa hali ya juu." alisisitiza Bw. Mkinga.

Aidha, Bw. Mkinga amesisitiza umuhimu wa watumishi kufungamana na taasisi washirika pamoja na wadau mbalimbali katika kutekeleza majukumu yao, huku akiwataka kuacha kufanya kazi kwa mazoea na badala yake kuzingatia taratibu kanuni na iliyopo miongozo katika utumishi wa umma.

Ameeleza ni muhimu watumishi kutoka ofisini na kwenda kuwahudumia wananchi moja kwa moja ili kuongeza ufanisi wa huduma zinazotolewa.

Sambamba na hilo, Bw. Mkinga ametoa wito kwa watumishi kufanya kazi kwa matokeo yanayoonekana na kuepuka udanganyifu katika mifumo ya kielekroniki ya upimaji utendaji kazi (PEPMIS) kwa kujaza taarifa sahihi.

Akizungumza kwa niaba ya Katibu Mtendaji wa THBUB, Mkurugenzi wa Utawala na Rasilimali Watu wa THBUB Bw. Jackson Nyamwihula, ameahidi kuwa THBUB itafanyia kazi kwa vitendo elimu iliyopatikana toka katika mafunzo hayo.



Bw. Oswin Henry Mkinga akizungumza na Watumishi wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora wakati wa Mafunzo ya e-Utendaji yaliyofanyika Ukumbi wa Jakaya Kikwete Jujini Dodoma Aprili 29, 2026

WATUMISHI WA UMMA WATAKIWA =KUIMARISHA UTENDAJI KAZI KWA MANUFAA YA WANANCHI DODOMA.



Mhe. Ridhiwani Kikwete (Mb)Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, akizungumza na Watumishi, Jijini Dodoma Juni 18, 2026.

Watumishi wa umma nchini wametakiwa kuimarisha utendaji kazi kwa kuzingatia uwajibikaji, uadilifu na weledi ili kuongeza tija katika utoaji wa huduma na kufanikisha azma ya Serikali ya kuwahudumia wananchi kwa ufanisi zaidi.

Wito huo umetolewa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. Ridhiwani Jakaya Kikwete (Mb) wakati wa uzinduzi wa Maadhimisho ya Wiki ya Utumishi wa Umma katika Viwanja vya Chinangali Park Jijini Dodoma Juni 17, 2026.

Akizungumza wakati wa uzinduzi huo, Mhe. Kikwete amesema maadhimisho hayo ni fursa ya kuongeza uelewa kuhusu huduma zinazotolewa na taasisi za umma, kuhamasisha matumizi ya mifumo ya utoaji huduma, kutoa huduma za papo kwa papo kwa wananchi na kupata mrejesho utakaosaidia kuboresha utendaji wa Serikali. Ameongeza kuwa maadhimisho hayo yanawapa watumishi wa umma nafasi ya kutafakari utekelezaji wa majukumu yao, kubadilishana uzoefu na kujifunza mbinu mpya za utoaji huduma kwa wananchi

Kaulimbiu ya maadhimisho hayo kwa mwaka 2026 ni "Kuchochea Uwajibikaji Jumuishi kwa Huduma Endelevu," inalenga kuimarisha uwajibikaji, uwazi na matumizi yenye tija ya rasilimali za umma. Amesisitiza kuwa Serikali itaendelea kuimarisha utumishi wa umma kupitia mageuzi ya kidijitali, usimamizi bora wa rasilimali watu, uongozi wenye kuwajibika na ushirikishwaji wa wananchi katika utoaji wa huduma.

Miongoni mwa taasisi zilizoshiriki katika maonesho hayo ni Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (THBUB), ambayo imeendelea kutoa elimu kwa wananchi kuhusu haki za binadamu na misingi ya utawala bora pamoja na kupokea na kushughulikia malalamiko mbalimbali kutoka kwa wananchi.

Akiongoza utoaji wa elimu kwa umma katika banda la THBUB, Mkurugenzi wa Idara ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, Bi. Suzan P. Ndeona, amesema wananchi wanaelimishwa kuhusu majukumu na huduma mbalimbali zinazotolewa na THBUB.

Ushiriki katika Maonesho ya Wiki ya Utumishi wa Umma unaakisi dhamira ya THBUB ya kusogeza huduma karibu na wananchi kwa kutoa elimu, kusikiliza changamoto zao na kuwaelekeza taratibu sahihi za kupata haki. Hatua hiyo inaunga mkono juhudi za Serikali za kujenga utumishi wa umma unaozingatia utawala bora.



Baadhi ya Watumishi wa THBUB wakiwa katika Maadhimisho ya Wiki ya Utumishi wa Umma Jijini Dodoma Juni 18, 2026

THBUB YAANZISHA KITENGO CHA TAASISI ZA HAKI JINAI KUIMARISHA UTOAJI HAKI.



Waziri wa Katiba na Sheria, Mhe.Dkt. Juma Zuberi Homera, (Mb) akiwa katika picha ya pamoja na Wakurugenzi na Wakuu wa vitengo wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (THBUB) katika viwanja vya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Jijini Dodoma, kabla ya kuanza kwa kikao cha uwasilishaji Bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2026/2027 Aprili 24, 2026.

Serikali imeanzisha Kitengo cha Taasisi za Haki Jinai ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa mapendekezo ya Tume ya Kuangalia Jinsi ya Kuboresha Taasisi za Haki Jinai Nchini. Hatua inayolenga kuimarisha usimamizi wa haki jinai na kuongeza ufanisi katika utoaji wa haki kwa wananchi.

Taarifa hiyo ameitoa Waziri wa Katiba na Sheria Dkt. Juma Zuberi Homera wakati akiwasilisha makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara yake kwa mwaka wa fedha 2025/2026 ambapo amesema kuwa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (THBUB) imefanya mapitio ya muundo wake na kuanzisha kitengo hicho ili kushughulikia masuala yanayohusu taasisi za haki jinai kwa ufanisi zaidi.

Dkt. Homera alisema kuwa Kitengo hicho tayari kimeanza kutekeleza majukumu yake ambapo, katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, kimepokea jumla ya malalamiko 69 yanayohusu ucheleweshwaji wa mashauri ya jinai, kunyimwa dhamana na matumizi mabaya ya madaraka.

Aidha, Malalamiko hayo yanaendelea kuchunguzwa na kufanyiwa kazi kwa mujibu wa sheria ili kuhakikisha haki inatendeka.

Waziri Homera ameongeza kuwa hatua hiyo inaoonesha dhamira ya Serikali ya kuendelea kuimarisha sekta ya haki jinai kwa kuboresha mifumo ya utendaji, kuimarisha ushirikiano wa taasisi na kuhakikisha haki za wananchi zinalindwa na kuheshimiwa kwa mujibu wa sheria.



Katibu Mtendaji wa Tume ya Haki za Bindamu na Utawala Bora Bw. Patience Ntwina (Kushoto), akifuatilia uwasilishwaji wa Bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria katika Ukumbi wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Aprili 24, 2026.

THBUB YAWEKEZA KWA WATUMISHI WAPYA ILI KUIMARISHA HUDUMA BORA KWA WANANCHI



Mkurugenzi wa Mipango na Bajeti, Bi. Regina Shashi (katikati), na Mhadhiri kutoka Chuo cha Utumishi wa Umma Tanzania, Bw. Fadhili Mtinda (kulia), wakiwa katika picha ya pamoja na watumishi wapya wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (THBUB) katika Ukumbi wa Chuo Cha Utumishi wa Umma Jijini Dodoma Juni 16, 2026.

Katika juhudi za kuendelea kujenga utumishi wenye weledi na ufanisi, Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (THBUB) imeendesha mafunzo elekezi kwa watumishi wapya 22 yaliyofanyika katika Chuo cha Utumishi wa Umma (TPSC), Dodoma kuanzia tarehe 16 hadi 19 Juni, 2026. Mafunzo hayo yalilenga kuwawezesha watumishi wapya kuelewa misingi ya utumishi wa umma, maadili ya kazi, sheria, kanuni na taratibu zinazoongoza utekelezaji wa majukumu yao.

Mafunzo hayo yalifunguliwa na Mkurugenzi wa Mipango na Bajeti, Bi. Regina Shashi kwa niaba ya Katibu Mtendaji wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora.

Bi. Regina aliwasisitiza watumishi ajira mpya kuzingatia maadili ya utumishi wa umma, kufanya kazi kwa uadilifu na kuwajibika katika kutekeleza majukumu waliyopewa.

“Mafunzo haya ni msingi wa kuwajengea watumishi wapya uelewa wa mazingira ya kazi, maadili ya utumishi wa umma na wajibu wao katika kutoa huduma bora kwa wananchi. Tunatarajia kila mshiriki ayatumie maarifa haya kuongeza ufanisi katika eneo lake la kazi.” — Amesema Bi Shashi. Katika mafunzo hayo, Washiriki walipata mafunzo kutoka kwa wawezeshaji mbalimbali, akiwemo Bw. Fadhili Mtinda (Mhadhiri) na Bi. Lilian Shio (Afisa Rasilimali Watu) kutoka Chuo cha Utumishi wa Umma, Bw. Nchimbi Morris, na Dkt. Raphael Tamilwai kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM).

Miongoni mwa mada zilizowasilishwa ni muundo wa Serikali na utekelezaji wa shughuli zake, maa-dili ya utumishi wa umma, utoaji wa huduma bora kwa wateja, Sheria ya Utumishi wa Umma Sura ya 298, mapitio ya Sheria ya Utumishi wa Umma Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2022, Kanuni za Kudumu za mwaka 2009, utunzaji wa kumbukumbu na nyaraka za Serikali, usalama wa taarifa, afya na lishe, elimu ya lishe na afya pamoja na elimu ya fedha na uwekezaji.

Mafunzo hayo pia yaliwapa washiriki nafasi ya kubadilishana uzoefu na kujenga mtandao wa ushirikiano baina ya watumishi wa THBUB. Mafunzo hayo yalihitimishwa na kufungwa na Kaimu Katibu Mtendaji, Bi. Suzan P. Ndeona na kukabidhi vyeti kwa washiriki. Akizungumza wakati wa kufunga mafunzo hayo, Bi. Ndeona aliwataka watumishi hao kuwa mabalozi wa maadili na utendaji bora katika maeneo yao ya kazi.

“Mafunzo haya yamewapa msingi mzuri wa kuanza safari ya utumishi wa umma. Tunaamini mtaya-tumia maarifa haya kuimarisha uwajibikaji, uadilifu na utoaji wa huduma bora kwa wananchi katika kila nafasi mtakayohudumu.” amesisitiza Bi. Ndeona



Kaimu Katibu Mtendaji wa THBUB, Bi. Suzan P. Ndeona akizungumza na watumishi wapya wakati wa mafunzo elekezi yaliyofanyika katika Ukumbi wa Chuo Cha Utumishi wa Umma Jijini Dodoma Juni 16, 2026.



Mhadhiri kutoka Chuo cha Utumishi wa Umma Tanzania, Bw. Fadhili Mtinda akiwasilisha mada kwa watumishi wapya wa THBUB wakati wa mafunzo elekezi yaliyofanyika katika Ukumbi wa Chuo Cha Utumishi wa Umma Jijini Dodoma Juni 16, 2026.

THBUB YASISITIZA ULINZI WA HAKI ZA BINADAMU KATIKA USIMAMIZI WA RASILIMALI ZA BAHARI.



Katibu mtendaji wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora Bw. Patience Ntwina akizungumza na wanawake wanaojihusisha na biashara ya mazao ya Bahari katika eneo la Feri kata ya Shangani Manispaa ya Mtwara Mikindani Juni 15, 2026.

Katika jitihada za kuhakikisha rasilimali za bahari zinawanufaisha wananchi kwa usawa na kuendelezwa kwa misingi ya haki za binadamu, Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (THBUB) imeendelea kutoa elimu kwa wadau wa sekta ya uvuvi kuhusu umuhimu wa kulinda haki za binadamu katika usimamizi na matumizi endelevu ya rasilimali hizo.

Akifungua mafunzo kwa wanufaika wa mazao ya rasilimali za bahari na wasimamizi wa rasilimali hizo yaliyofanyika Msanga Mkuu mkoani Mtwara Juni 15, 2026, Katibu Mtendaji wa THBUB, Bw. Patience Ntwina, amesema maendeleo ya sekta ya bahari hayawezi kupatikana bila kuwepo kwa mazingira yanayoheshimu haki za binadamu na utawala bora.

Ameeleza kuwa kila mdau anapaswa kutambua haki zake na kutekeleza wajibu wake ili kuhakikisha matumizi ya rasilimali za bahari yanakuwa endelevu na yenye manufaa kwa vizazi vya sasa na vijavyo.

Bw. Ntwina amesisitiza kuwa usimamizi wa rasilimali za bahari unapaswa kuwalinda wavuvi wadogo na jamii za pwani, ambazo ndizo zinazoitegemea sekta hiyo kwa maisha yao ya kila siku. Katika taarifa yake amesema haki ya kushiriki katika matumizi ya rasilimali za asili, kupata taarifa sahihi na kushirikishwa katika maamuzi ni miongoni mwa misingi muhimu ya utawala bora inayochochea maendeleo ya wananchi na taifa kwa ujumla.

Mafunzo hayo, yanayotekelezwa katika mikoa ya Mtwara, Lindi, Pwani na Tanga, yanalenga kuwajengea uwezo wadau kuhusu usimamizi endelevu wa rasilimali za bahari, sheria zinazosimamia sekta hiyo pamoja na namna ya kutambua na kuripoti vitendo vinavyoweza kusababisha ukiukwaji wa haki za binadamu. Washiriki pia wanapata nafasi ya kujadili changamoto zinazowakabili katika shughuli zao za kiuchumi na kupendekeza suluhisho linalozingatia maslahi ya jamii na taifa.

Akizungumzia taarifa ya uchambuzi wa awali uliofanywa na THBUB, Bw. Ntwina amesema takwimu zinaonesha wavuvi wadogo wana mchango mkubwa katika kuimarisha usalama wa chakula, kuongeza kipato cha kaya, kuzalisha ajira na kukuza uchumi wa maeneo ya pwani. Aidha, alisema sekta ya uvuvi ina nafasi muhimu katika kuhifadhi utamaduni wa jamii za pwani na kuimarisha mshikamano wa kijamii.

Kwa upande wake, Mkuu wa Kitengo cha Utafiti kutoka Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Bw. Fundikila Wazambi, aliwahimiza washiriki kufahamu kuwa haki za binadamu huenda sambamba na wajibu. Alisisitiza kuwa kila mvuvi anatakiwa kutambua mipaka ya haki zake na kuhakikisha shughuli zake hazikiuki haki za wengine.

Nao washiriki wa mafunzo hayo kwa nyakati tofauti wameeleza kuwa elimu waliyoipata imewaongezea uelewa kuhusu haki zao na wajibu wao katika sekta ya uvuvi. Wamesema maarifa hayo yatawasaidia kutambua mapema viashiria vya ukiukwaji wa haki za binadamu, kuwasilisha malalamiko kwa mamlaka husika na kushiriki kikamilifu katika usimamizi endelevu wa rasilimali za bahari.

Kupitia programu hiyo, THBUB inaendelea kuhamasisha jamii kuhusu ulinzi na ukuzaji wa haki za binadamu katika sekta mbalimbali za maendeleo.

THBUB YA ZINDUA BUSTANI YA MITI WIKI YA MAZINGIRA.



Mkurugenzi wa Haki za Binadamu kutoka Wizara ya Katiba na Sheria Bi. Nkosari Sarakikya, akipanda mti katika bustani ya THBUB, eneo la Nkuhungu, Jijini Dodoma Juni 5, 2026.

Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (THBUB) imezindua bustani ya miti katika Mtaa wa Salama, Kata ya Nkuhungu, Jijini Dodoma ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya Wiki ya Mazingira.

Akizungumza katika hafla hiyo Juni 04, 2026 kwa niaba ya Waziri wa Katiba na Sheria, Mkurugenzi wa Haki za Binadamu kutoka Wizara ya Katiba na Sheria, Bi. Nkosori

Sarakikya, amesema kuwa haki za binadamu na mazingira ni mambo yanayohusiana moja kwa moja na hayawezi kutenganishwa.

"Kulinda mazingira ni kulinda haki za binadamu, na kulinda haki za binadamu yapasa kuendana na kuhifadhi mazingira," amesema Bi. Sarakikya. Pia alisisitiza kuwa mazingira safi, salama na endelevu ni haki ya msingi ya binadamu inayotambulika kitaifa na kimataifa.

Kwa upande wake, Katibu Mtendaji wa THBUB, Bw. Patience Ntwina amesema uzinduzi wa bustani hiyo unaonesha kwa vitendo namna THBUB inavyotekeleza jukumu lake la kuhamasisa hifadhi ya haki za binadamu na misingi ya utawala bora kupitia shughuli za utunzaji wa mazingira.

"tunayo furaha kubwa sana siku ya leo, si kwa sababu ya bustani pekee, bali kwa sababu shughuli hii inaonesha namna haki za binadamu zinavyofungamana na mazingira tunayoyaishi kila siku."amesema Bw. Ntwina

Bw. Ntwina amesema bustani hiyo ni sehemu ya juhudi za THBUB katika kuchangia ustawi wa jamii na kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi.

Akizungumza kwa niaba ya wananchi wa eneo hilo, Mwenyekiti wa Mtaa wa Salama, Bw. Habasi Mwijuki amesema bustani hiyo imebadilisha sura ya eneo hilo ambalo hapo awali lilikuwa kame na lisilovutiana kufanya kuwa sehemu ya kupumzika kwa wakazi wengi wa eneo hilo.

Uzinduzi wa bustani hiyo ni shughuli iliyotekelezwa kama sehemu ya matukio kuelekea kilele cha Siku ya Mazingira Duniani ambayo huadhimishwa Juni 5 kila mwaka.



Mkurugenzi wa Haki za Binadamu kutoka Wizara ya Katiba na Sheria Bi. Nkosori Sarakikya akizindua Bustani ya THBUB eneo la Nkuhungu kwa Swai akiwa na Katibu Mtendaji wa THBUB Bw. Patience Ntwina Juni 5, 2026.



Watumishi wa THBUB wakifanya usafi wa mazingira katika Bustani ya THBUB, eneo la Nkuhungu Jijini Dodoma, Juni 5, 2026.

WATUMISHI WATAKIWA KUFANYA KAZI KWA BIDII



Katibu Mtendaji wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora Bw. Patience Ntwina akitoa neno katika kuadhimisha Siku ya Wafanyakazi Duniani Jijini Dodoma 2026.

Katibu Mtendaji Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, Bw. Patience Ntwina ametoa wito kwa watumishi kufanya kazi kwa bidii ili kujikwakumua kiuchumi.

"Uchumi imara, shindani na endelevu hauwezi kutokea katika mazingira yetu na kufikia Dira ya Taifa 2050 kama hatutafanya kazi kwa bidii" amesema Bw. Ntwina.

Kauli hiyo ameitoa wakati wa mahojiano na vyombo vya habari yaliyofanyika baada ya sherehe za maadhimisho ya Siku ya Wafanyakazi Duniani kimkoa katika Uwanja wa Jamhuri Jijini Dodoma Mei Mosi, 2026.

Katika kuadhimisha siku hiyo Watumishi wa THBUB katika matawi ya Dar es Salaam, Mtwara, Tabora na Mwanza waliungana na Wafanyakazi wengine wa mikoa hiyo kusherehekea siku hiyo.

Katika Mkoa wa Dodoma, Mkuu wa Mkoa wa Dodoma Mhe. Senyamule amewataka waajiri wote Serikalini na sekta binafsi kuhakikisha kuwa wafanyakazi wanafaya kazi kwa kuzingatia sheria na taratibu zilizowekwa na waajiri wahakikishe wanapeleka tabasamu kwa watumishi ili kwenda sambamba na kauli ya Mhe. Rais Samia Suluhu Hassan kwa watumishi kupeleka huduma bora kwa wananchi

Katika Mkoa wa Dar es Salaam maadhimisho hayo yalifanyika katika Viwanja vya Mnazi Mmoja jijini Dar es Salaam,

ambapo katika hafla hiyo Mgeni rasmi alikuwa Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam Mhe. Albert Chalamila ambaye katika hotuba yake amewataka waajiri nchini kuzingatia maslahi ya wafanyakazi kwa kuwapatia haki zao stahiki pamoja na kuhakikisha wanakuwa na mazingira bora ya kazi.

Kwa/ upande wa Mkoa wa Mwanza, Maadhimisho hayo yameongozwa na Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Mhe. Said Mtanda ambaye alikuwa mgeni rasmi. Mhe. Mtanda aliwataka wafanyakazi kuendelea kufanya kazi kwa bidii, uadilifu na uzalendo ili kuongeza tija katika utekelezaji wa majukumu yao pamoja na kuchochea maendeleo ya taifa.

Na kwa upande wa Zanzibar THBUB iliishiriki kilele cha maadhimisho hayo katika viwanja vya Nanenane vilivyopo Dole, Kizimbani Wilaya ya Magharibi A, Mkoa wa Mjini Magharibi na mgeni rasmi akiwa ni Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mhe. Dk. Hussein Ali Mwinyi.

Maadhimisho ya Siku ya Wafanyakazi kwa mwaka 2026 yalibebwa na Kauli mbiu isemayo "Kazi zenye staha ni nguzo imara kwa maendeleo endelevu katika utekelezaji wa Dira ya Taifa 2050."



Baadhi Watumishi wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora Makao Makuu wakiwa katika kilele cha Siku ya Wafanyakazi Duniani Jijini Dodoma Mei 1, 2026.



Baadhi ya Wafanyakazi wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora Tawi la Dar es Salaam wakiwa katika Viwanja vya Mnazi Mmoja Jijini Dar es Salaam wakati wa maadhimisho ya Siku ya Wafanyakazi Duniani Mei 1, 2026.

THBUB YASULUHISHA MGOGORO WA MAZISHI, YAWEZESHA MAREHEMU JACKSON KYAGALA KUZIKWA NYUMBANI MULEBA



Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (THBUB) imefanikiwa kutatua mgogoro wa mazishi uliokuwa umechelewesha mazishi ya marehemu Jackson Johanes Kyagala, hatua ili-yowezesha mwili wake kusafirishwa na kuzikwa nyumbani kwao Wilaya ya Muleba, mkoani Kagera, baada ya siku kadhaa za sintofahamu.

Mgogoro huo ulitokana na kutokuwepo kwa mwafaka kati ya baba mzazi wa marehemu, Johanes Modest Kyagala na mwajiri wa marehemu, Osmond Tumainiel Moshia, kuhusu eneo la mazishi pamoja na taratibu za kuukabidhi mwili kwa familia.

THBUB ilipokea lalamiko hayo kupitia Dawati la Malalamiko tarehe 26 Mei, 2026, baada ya mwili wa marehemu kuhifadhiwa kwa siku kadhaa katika Hospitali ya Rufaa ya Kilimanjaro Christian Medical Centre (KCMC), Moshi.

Baada ya kupokea malalamiko hayo, THBUB ilianza mchakato wa usuluhishi kwa kufanya mazungumzo na pande zote zilizohusika. Kupitia mazungumzo hayo, ilipatikana suluhu iliyomwezesha baba mzazi wa marehemu pamoja na ndugu mwingine kusafiri kwenda Arusha kwa ajili ya kuutambua mwili.

Baada ya utambuzi huo kufanyika, mwajiri wa marehemu alikubali kugharamia usafirishaji wa mwili kutoka Arusha hadi Muleba, ambapo marehemu alizikwa kwa heshima mbele ya familia, ndugu na jamii yake.

Hii inaonesha nafasi na umuhimu wa THBUB katika kutatua migogoro kupitia usuluhishi na kulinda utu na heshima ya binadamu.

HABARI PICHA



Mkurugenzi Msaidizi wa Rasilimali Watu, Bw. Johnston Mwakalitolo akifungua mafunzo elekezi kwa watumishi wapya wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (THBUB) yaliyofanyika katika ukumbi wa Chuo cha Utumishi wa Umma Juni 15, 2026



Viongozi na Watumishi wa THBUB wakifanya shughuli za usafi wa mazingira katika Bustani ya THBUB iliyopo Mtaa wa Salama, Kata ya Nkuhungu Jijini Dodoma, ikiwa ni sehemu ya maandalizi kuelekea maadhimisho ya siku ya mazingira Duni-ani Juni 4, 2026

HABARI PICHA



Afisa wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora Tawi la Tabora, Bw. Raphael Mavunde, akitoa elimu kuhusu haki za binadamu na misingi ya Utawala Bora katika Jukwaa la Tatu Vyama vya Ushirika wa Maendeleo lililofanyika Wilayani Kaliua, Mkoa wa Tabora Aprili 29, 2026



Baadhi ya Watumishi wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (THBUB) ofisi ya Zanzibar, wakiwa katika viwanja vya Dole Mkoa wa Mjini Magharibi Zanzibar, wakati wa maadhimisho Siku ya Wafanyakazi Duniani Mei 1, 2026.

HABARI PICHA



Baadhi ya watumishi wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (THBUB), wakifuatilia mafunzo maalum ya e-utendaji (Mobile Clinic) yaliyolenga kuimarisha utendaji kazi, maadili ya utumishi wa umma pamoja na mshikamano kazini katika Ukumbi wa Jakaya Kikwete Aprili 29, 2026



Bw. Oswin Henry Mkinga akitoa mafunzo maalum ya e-utendaji (Mobile Clinic) kwa Watumishi wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (hawapo pichani), yaliyolenga kuimarisha utendaji kazi, maadili ya utumishi wa umma pamoja na mshikamano kazini katika Ukumbi wa Jakaya Kikwete Aprili 29, 2026,

HABARI PICHA



Wakazi wa Shinyanga na maeneo ya jirani wakipatiwa elimu kuhusu haki za binadamu na utawala bora wakati walipotembelea banda la THBUB wakati wa Kampeni ya Msaada wa Kisheria wa Mama Samia Shinyanga Mei 12, 2026.



Waziri wa Katiba na Sheria Mhe. Dkt. Juma Homera (Mb) (Watatu kushoto) akimkabidhi vitendea kazi (Magari) Katibu Mtendaji wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, Bw. Patience Ntwina katika hafla iliyofanyika Mtumba, Jijini Dodoma Aprili 15, 2026.